**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 23222761-5
*Fax No.* +255 026 2322624
**E-mail:** cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

# TAARIFA KWA UMMA

Spika wa Bunge Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb) amemwandikia Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Jaji Jacob Mwambegele barua ya kumuarifu kuwepo kwa nafasi moja wazi ya kiti cha Ubunge Viti Maalum Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Spika ameandika barua hiyo kufuatia kupokea barua ya kujiuzulu kutoka kwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo juzi tarehe 17 Agosti, 2023.

Mheshimiwa Bahati amejiuzulu nafasi hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 149 (1) (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Katika barua yake kwa Mheshimiwa Spika, ameeleza sababu za kujiuzulu ni kuangalia namna nyingine ya kuwatumikia Watanzania katika Bunge.

" ...Ninakusudia kushiriki kwenye mchakato wa Uchaguzi Mdogo wa nafasi ya Ubunge wa Jimbo la Mbarali unaotarajia kufanyika siku za hivi karibuni." inaeleza sehemu ya barua hiyo.

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na
Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 941,
**DODOMA**.

19 Agosti, 2023.